



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Ofisi ya UNBoA, New York, Marekani.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (CAG) Prof. Mussa Juma Assad leo tarehe 24 Julai, 2018 amekabidhi nafasi yake ya Ujumbe wa Bodi ya Ukaguzi ya Umoja wa Mataifa (UNBoA) kwa nchi ya Chile. Makabidhiano hayo yamefanyika kwenye Ukumbi wa Mikutano uliopo kwenye jengo la Makao Makuu ya Umoja wa Mataifa, Jijini New York nchini Marekani baada ya Tanzania kumaliza muda wake wa kipindi cha miaka sita (6) kuanzia Julai Mosi, 2012.

Pamoja na kufanya makabidhiano hayo, CAG Prof. Assad pia amehudhuria Kikao cha Kawaida cha 72 cha Bodi hiyo na kuwasilisha jumla ya ripoti 13 za Ukaguzi wa Mashirika ya Umoja wa Mataifa (UN). Ripoti hizo 13 zilizowasilishwa na Prof. Assad na kutiwa saini na wajumbe wa Bodi ya Ukaguzi ya UN ni pamoja na Ukaguzi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Maendeleo (UNDP), Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA), Shirika la Umoja wa Mataifa la Misaada kwa Wakimbizi wa Palestina na Mashariki (UNRWA), Mfuko wa Akiba kwa Watumishi wa UNRWA Wakazi (UNRWA – SPF), Shirika la Umoja wa Mataifa la Masuala ya Wanawake (UN – Women) na Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Mazingira (UNEP).

Ripoti nyingine ni za Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Mazingira ulio chini ya UNDP-GEF, Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Mazingira ulio chini ya Shirika UNEP-GEF, Mfuko wa Mikopo Midogo midogo ulio chini ya UNRWA - MD Shirika la Umoja wa Mataifa la Makazi (UN Habitat), Shirika la Umoja wa Mataifa la Ukuzaji Mitaji (UNCDF), Mahakama ya Umoja wa Mataifa inashughulikia Mauaji ya kimbari ya Yugoslavia ya zamani (ICTY), pamoja na ripoti ya Mpango wa Kupunguza Shughuli za Mahakama za Kimataifa Zinazoshughulikia Mauaji ya Kimbari (MICT).


Akizungumza baada ya kuwasilisha ripoti zake, Prof. Assad amesema kikao hicho ni cha mwisho kwa nchi ya Tanzania kuhudhuria kama Mjumbe wa Bodi ya UNBoA na kinatarajiwa kuhitimishwa kesho tarehe 25 Julai, 2018. Hata hivyo, Prof. Assad amefafanua kuwa Tanzania itaendelea kuwa mjumbe mwangalizi "Observer Member" kwenye Jopo la Wakaguzi wa Nje wa Umoja wa Mataifa kwa kipindi cha miaka miwili mfululizo baada ya kung'atuka kwenye nafasi ya Ujumbe wa Bodi hiyo.

Prof. Assad amesema, katika kipindi cha miaka sita ya UNBoA, Tanzania haikuwa tu Mjumbe wa UNBoA bali pia ilipata fursa ya kuongoza Bodi ya Ukaguzi wa Umoja wa Mataifa (UNBoA) kwa kipindi cha miaka miwili (2).

"Nimekuwa mwenyekiti wa UNBoA kwa miaka miwili mfululizo kuanzia Januari Mosi, 2015 hadi 31 Desemba, 2016 ambapo nimekuwa na jukumu la kuwasilisha taarifa za UNBoA katika Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kupitia Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Nilitumia fursa hiyo kumshauri Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kwa niaba ya UNBoA njia bora ya kuimarisha mifumo ya udhibiti katika usimamizi wa fedha pamoja na kubadili muda wa uwasilishaji wa hesabu za Mashirika ya Umoja wa Mataifa ambayo yanatoa hesabu zake mwishoni mwa mwezi Aprili", amesema CAG Prof. Assad.

Tanzania inaingia katika historia ya dunia kuwa nchi ya kwanza katika Ukanda wa Afrika Mashariki na ya tatu (3) Barani Afrika kuteuliwa mjumbe wa Bodi ya Ukaguzi wa Umoja wa Mataifa (UNBoA) tangu kuanzishwa kwa Bodi hiyo mwaka 1946. Nchi nyingine za Afrika ambazo zimewahi kuwa wajumbe wa Bodi ya Ukaguzi ya Umoja wa Mataifa ni Ghana na Afrika ya Kusini tu.

Tanzania imekuwa mjumbe wa Bodi hiyo kuanzia Julai Mosi, 2012 hadi tarehe 30 Juni, 2018 baada ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuteuliwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kuwa mjumbe wa Bodi hiyo mnamo tarehe 11 Novemba, 2011, kwenye Kikao cha 58 cha Baraza hilo. Tanzania ilishirikiana na wajumbe wengine wa Bodi kutoka nchi za Uingereza, China, Ujerumani na India kwa vipindi tofauti.



Sarah Reuben

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini (GCU)

24 Julai, 2018